TUME YA KIKRISTO YA HUDUMA ZA JAMII

KAMATI YA MITIHANI YA PAMOJA KANDA YA KASKAZINI

MTIHANI WA UPIMAJI – KIDATO CHA PILI, AGOSTI 2026

021 KISWAHILI

MUONGOZO WA USAHIHISHAJI

1. MAJIBU (ALAMA 10)

i.	ii.	iii.	iv.	v.	vi.	vii.	viii.	ix.	x.
B	C	B	D	A	B	B	D	D	E

2. MAJIBU (ALAMA 05)

SAFU A	i.	ii.	iii.	iv.	v.
SAFU B	D	E	C	F	B

3. Mtahiniwa anatakiwa asome habari aliyopewa kisha ajibu kulingana na maswali (ALAMA 10)
   i. Kichwa cha habari aandike kwa herufi kubwa na kupigia mstari (ALAMA 02)
   UZINDUZI WA MABWENI
   MRADI WA MABWENI
   ii. Mtahiwa anatakiwa aandika sababu mbalimbali zilizopelekea wanakijiji kujenga mabweni (ALAMA 01) 0.5@
      a) Wanafunzi walitumia muda mrefu kufika shuleni
      b) Uwepo wa changamoto mbalimbali uliokatisha masomo ya wanafunzi kama vile utoro, uvutaji bangi na kujihusisha katika makundi mabaya
   iii. Mtahaniwa anatakiwa aandike visawe vya maneno yafuatayo(ALAMA 01) 0.5@
      (a) Wasichana- banati, binti, mwanamwali, warembo,
      (b) Wavulana- maghulamu, janadume, mtanashati
   iv. Mtahaniwa anatakiwa aandike methali moja kulingana na habari aliyosoma; (ALAMA 01)
      - Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
      - Kidole kimoja hakivunji chawa
   v. Mtahaniwa anatakiwa afupishe habari kulingana na maelekezo yafuatayo (ALAMA 05)
      - Kichwa cha ufupisho – Herufi kubwa na apigie mstari (ALAMA 01)
      - Atumie maneno yake mwenyewe bila kutoka nje ya lengo (ALAMA 01)
      - Aanze kwa aya (ALAMA 01)
      - Awe na mtiririko mzuri wa maneno pamoja na kuzingatia idadi ya maneno aliyopewa (ALAMA 02)

4. Mwanafunzi anatakiwa kuandika hoja za umuhimu wa matumizi ya Kiswahili (ALAMA 10) 02@
   i. Lugha ya Kiswahili inatumika kuunganisha watanzania wote.
   ii. Lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi inatumika katika shughuli mbalimbali kama vile kisiasa, kiuchumi, kielimu na kiutamaduni.
   iii. Hutumika kama utambulisho wa taifa letu.
   iv. Inatumika kufundishia masomo yote katika shule za msingi na vyuo vya ualimu vinavyotumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia, pia Kiswahili hutumika kama somo katika elimu ya sekondari na vyuo vikuu.
   v. Inachangia katika kukuza uchumi, amani na utulivu nchini Tanzania.
   vi. Inatumika kutoa fursa ya ajira.

5. Mwanafunzi anatakiwa aeleze taarifa zinazopatikana kwenye matini ya kamusi (ALAMA 10) 02@
   i. Huonesha asili ya neno/ etimolojia
      Mfano. Neno "ngeli" asili yake ni kibantu
   ii. Maana au fasili ya neno
      Mfano. Mama – mzazi mwenye jinsia ya kike
   iii. Matamshi sahihi ya maneno
      Mfano. Neno "bundi" -/'*bundi*/
   iv. Huonesha kategoria ya neno au aina ya neno.
      Mfano. Cheza- *Kitenzi(kt)*
   v. Huonesha ngeli za nomino
      Mfano. Bundi /a-wa/
   vi. Inaonesha umoja na wingi wa neno
      Mfano. Mti- miti
   vii. Huonesha visawe vya maneno
      Mfano. Msichana-binti

6. Mtahiniwa anatakiwa atunge sentensi zenye umoja na wingi kulingana na ngeli alizopewa (ALAMA 10) 02@
   i. Ngeli ya LI-YA
      - Gari limepinduka – magari yamepinduka
   ii. Ngeli ya U-ZI
      - Uzi umefumuka – nyuzi zimefumuka
   iii. Ngeli ya I-ZI
      - Nguo yake imechafuka – nguo zake zimechafuka
   iv. Ngeli ya KU
      - Kucheza kwake kunafurahisha
   v. Ngeli ya PA-MU-KU
      - Hapa panapendeza
      - Mahali mule mnapendeza
      - Kule kunapendeza

7. Mtahiniwa anatakiwa kuandika aina ya sentensi na muundo wake. Sentensi ya kwanza imefanyika kama mfano. (ALAMA 10) 02@
   i. Sisi tunasoma kitabu. **Aina – sentensi sahili**

      Muundo- kishazi huru kimoja/ kitenzi kikuu kimoja
   ii. Aina – sentensi ambatani

      Muundo- imejengwa na sentensi sahili mbili
   iii. Aina – sentensi changamani

      Muundo- viambishi vya masharti
   iv. Aina- sentensi sahili

      Muundo- kishazi huru kimoja chenye kitenzi kishirikishi
   v. Aina -Sentensi ambatani

      Muundo- sentensi changamani moja na sahili moja
   vi. Aina- sentensi sahili

      Muundo- kishazi huru kimoja chenye vitenzi visaidizi viwili na kitenzi kikuu kimoja
8. Mtahiniwa anatakiwa kutoa maana ya rejesta na kutaja mtindo wa lugha uliotumika katika sentensi alizopewa (ALAMA 10) 02@
   (a) Rejesta – ni mtindo wa lugha unaotumika kulingana na shughuli na mahali mahususi mfano. Mtindo wa lugha unaotumika hospitalini, shuleni, mahakamani, kanisani au shambani hutofautiana.
   (b) Mtahiniwa anatakiwa ataje mazingira yaliyotumika katika sentensi alizopewa
      i. Hospitalini
      ii. Gulioni/ sokoni/mnadani
      iii. Bungeni
      iv. Mahakamani

9. Mtahiniwa anatakiwa kusahihisha sentensi kwa usahihi (ALAMA 10)2@
   i. Mwenyekiti wa mtaa alisisitiza usafi wa mazingira.
   ii. Serikali ya jamuhuri ya muungano wa Tanzania inasisitiza umoja.
   iii. Wote walilala vizuri.
   iv. Musa huwa anaenda kanisani/ Musa huenda kanisani.
   v. Walimu wamekunywa chai

10. Mtahiniwa anatakiwa aandike insha inayohusu chanzo cha mmomonyoko wa maadili

Mgawanyo wa alama. Kichwa Cha Insha - (alama 02)

Utangulizi- (alama 02)

Kiini - hoja tano(alama10@02)

Hitimisho -(alama 01) jumla 15

Jibu:

Mmomonyoko wa maadili hiki ni kitendo cha kuporomoka au kupungua kwa maadili mema katika jamii au kwa mtu binafsi kwa kushindwa au kuacha kufuata kanuni, Mila na desturi za jamii husika.

Chanzo Cha Mmomonyoko wa maadili.

i. Ushawishi wa marafiki/ makundi rika/ makundi mabaya. Vijana huiga au kushirikiana kufanya mambo mabaya ili kukubalika.

ii. Vyombo vya habari/. Vijana huiga tabia mbaya katika mitandao ya kijamii, filamu au miziki inayoonyesha mambo yasiyofaa.

iii. Malezi duni/hafifu kwa watoto. Watoto wanaokosa malezi ya wazazi huangukia katika mmomonyoko wa maadili kwani hukosa uangalizi na muongozo sahihi.

iv. Umaskini. Watu hufanya vitendo visivyofaa mf: wizi, rushwa na kujiuza miili yao ili kupata kipato kwa ajili ya kuendesha maisha yao.

v. Utandawazi. Watu huiga utamaduni wa kigeni na kuacha mila na desturi za jamii zao

vi. .Kutozingatia misingi ya dini. Kukosa hofu ya Mungu au kupuuza mafundisho ya dini.

vii. Migogoro ya kifamilia.

viii. Ukosefu wa elimu.

ix. Tamaa.